JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Mtaa wa Utumishi 10 Mtumba, S.L.P. 1074, 41207 DODOMA. Nambari ya simu: 026-2610780,
Barua pepe: secretary@psc.go.tz, Tovuti: www.psc.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

Tume ya Utumishi wa Umma ni chombo rekebu kilichoanzishwa chini ya Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 (Marejeo ya Mwaka 2023) chenye wajibu wa kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo.

Majukumu ya msingi ya Tume yameainishwa katika Kifungu cha 12(1) cha Sheria hiyo na yamegawanyika katika maeneo makuu matatu (3) ambayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kutoa Ushauri;
(b) Urekebu; na
(c) Kusimamia Utoaji wa Haki.

Tume itafanya Mkutano wake wa kwanza kwa Mwaka wa Fedha **2026/2027** chini ya Mwenyekiti wake **Jaji (Mst.) Hamisa H. Kalombola** kwa muda wa wiki nne kuanzia tarehe **21/09/2026** hadi tarehe **16/10/2026.** Mkutano huo utafanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Umma, zilizopo katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.

Katika Mkutano huu,Tume itajadili na kutoa uamuzi wa Rufaa na Malalamiko mbalimbali yaliyowasilishwa na Watumishi wa Umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka zao za Nidhamu. Hii ni kwa mujibu wa Vifungu vya **12(1)(d)** na **27(1)(b**) vya Sheria

Katika Mkutano huo, Tume itafanya ziara kwenye Taasisi tisa (9) za Serikali zilizopo katika Mkoa wa Dodoma kwa lengo la kutoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira, Mamlaka za Nidhamu na Watumishi wa Umma ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa jukumu lake la Urekebu.

Pamoja na taarifa ya Mkutano huu, napenda kutoa taarifa kuwa Tume inaendelea na Zoezi la Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria katika Usimamizi wa Utumishi wa Umma lililozinduliwa na Mhe. Ridhiwani J. Kikwete (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe 10/08/2026 jijini Dar-es-Salaam ambapo Taasisi za Serikali **300** zitakaguliwa. Hadi kufikia tarehe 17/09/2026, Tume imeshakagua Taasisi **97** na inategemea kukamilisha ukaguzi huu tarehe 19/12/2026.

IMETOLEWA NA:

Nolasco J. Kipanda
KATIBU
TUME YA UTUMISHI WA UMMA

18/09/2026